

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**MKOA WA DAR ES SALAAM**

Anwani ya Simu:  
Simu: 2203156/58  
Fax: +25522203213  
Tovuti: [www.dsm.go.tz](http://www.dsm.go.tz)  
Barua Pepe: [ras@dsm.go.tz](mailto:ras@dsm.go.tz)



**OFISI YA MKUU WA MKOA**  
**3 Barabara ya Rashidi**  
**Kawawa,**  
S.L.P 5429,  
**12880 -DAR ES SALAAM.**  
**Tanzania**

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

**UJENZI WA OFISI ZA WALIMU DAR ES SALAAM SASA KUANZA RASMI**

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mheshimiwa Paul Makonda leo amezindua rasmi zoezi la ufyatuuji wa Matofali kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi za kisasa 402 za Walimu ambapo amewasihi wadau na wananchi kuunga Mkono jitihada hizo.

Katika uzinduzi huo Mhe. Makonda ameshiriki zoezi la ufyatuuji wa Matofali kwa ajili ya Ujenzi huo.

Mhe. Makonda amesema lengo la Ujenzi wa Ofisi hizo ni kuboresha Mazingira ya kufanya kazi kwa walimu ili waweze kutoa elimu bora kwa wanafunzi na kuongeza ufaulu.

Amesema wapo wengi waliopanga kufanya ujenzi wa Ofisi za Walimu lakini mipango hiyo iliishia kubaki kwenye makarabrasha maofisini lakini kupitia juhudi zake na Kamati aliyoiunda wameweza kuleta matokeo chanya.

RC Makonda ametoa wito kwa wananchi na wadau kuchangia mabati, saruji, kokoto, mchanga, nondo au nguvu kazi ili kuwawezesha walimu kufanyakazi katika mazingira bora.

Amesema hataki kuona kwenye Mkoa wake walimu wanadhaliika kwa kukosa ofisi na vyoo hali inayopelekea kujisaidia kwa majirani, bar au vichakani.

Aidha amesema hadi sasa amefanikiwa kupata mifuko zaidi ya 10,000 ya saruji mashine za kufyatulia matofali, gurdoza na vifaa vingine ambapo ataendelea kugonga hodi kwa wadau ili waweze kuchangia ujenzi huo.

Amewaomba Wananchi kuwa na uzalendo kwa kujitoa katika ujenzi huo iwe kwa mtu binafsi au Vikundi vya Joaging, Timu za Mpira na vikundi vya maendeleo.

Ameipongeza Kamati ya ujenzi wa Ofisi za walimu, JKT, Jeshi la Magereza, Jeshi la Polisi, NHC, TBA, Channel Ten na Umoja wa Wamiliki wa Malori na wengine kwa namna wanavyojitoa kusaidia katika zoezi hilo.

Katika hatua nyingine RC Makonda amesema atatoa TV 30 kwa Magereza ya Ukonga, Segerea na Keko ili wafungwa wapate fursa za kutazama hotuba za Rais DR.JOHN MAGUFULI ili wajue maendeleo yanayofanyika uraiiani.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Kamati ya Ujenzi wa Ofisi za Walimu Canal Charles Mbuge amesema hadi sasa kiasi cha fedha kilichotumika ni zaidi ya Million 200 ambapo watahakikisha ujenzi huo unakamilika.

Imetolewa na:-

Kitengo cha Habari na Uhusiano

**OFISI YA MKUU WA MKOA**

**DAR ES SALAAM**

19/09/2017